

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA MULEBA



Kumb.Na.KGR/MLB/HW/I.9/172

20 Machi, 2024

TANGAZO LA KUUZA VIWANJA.

MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MULEBA ANAWATANGAZIA WANANCHI, MAKAMPUNI NA TAASISI ZOTE ZENYE NIA YA DHATI YA KUWEKEZA WILAYANI MULEBA KATIKA SEKTA YA VIWANDA, HOTELI NA HUDUMA YA KITUO CHA MAFUTA, KUWA HALMASHAURI INAUZA VIWANJA KATIKA ENEO LA MAGATA, KILOMETA MOJA TOKA MULEBA MJINI, PEMBEZONI MWA BARABARA KUU IENDAYO BIHARAMULO NA CHATO.

2. BEI ZA VIWANJA NI KAMA IFUATAVYO;-

NA	MATUMIZI	BEI KWA MITA MOJA YA MRABA (TSHS)
1.	Viwanda	2,000
2.	Kituo cha mafuta	10,000
3.	Hoteli	2,000

3. Fomu za maombi zinapatikana katika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) kitengo cha ardhi, Halmashauri ya wilaya ya Muleba.

4. Fomu italipiwa Tshs 20,000 kwa kila ombi la kiwanja, gharama za maombi hazirudishwi.

5. Fomu zitaanza kutolewa toka siku ya tarehe ya tangazo hili na mwisho wa kupokea fomu za maombi ni tarehe 10/4/2024

6. Mwombaji atakaepata kiwanja atawajibika kusaini mkataba maalum wa uendelezaji wa kiwanja, ambapo ndani ya mkataba huo atalazimika kuendeleza kiwanja atakachopewa ndani ya miezi 36 toka tarehe ya malipo.

7. Waombaji watakaopata viwanja watatangazwa katika mbao za matangazo na watawajibika kulipia viwanja ndani ya kipindi cha siku 28 toka tarehe ya tangazo la kupewa kiwanja. Vinginevyo kiwanja kitagawiwa kwa mwombaji mwingine mwenye sifa.

TAFADHALI UTAPOSOMA TANGAZO HILI WAJULISHE WENGINE.


Christina Akyoo

**/MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MULEBA**

